
WRBWB
WAMI/RUVU BASIN WATER BOARD

WIZARA YA MAJI

BODI YA MAJI BONDE LA WAMI/RUVU

UTABIRI WA HALI YA WINGI WA MAJI KATIKA MTO RUVU KWA KIPINDI CHA SIKU 10 KUANZIA TAREHE 6 NOVEMBA HADI 16 NOVEMBA, 2026







Imeandaliwa na;

Bodi ya Maji Bonde la Wami/Ruvu

P.O. Box 826, Morogoro—Tanzania
Phone: 0800114031 / 0800114032
E-mail: barua@wrbwb.go.tz
Website: www.wrbwb.go.tz


Novemba, 2026

1. UTANGULIZI

Yaliyomo

1. UTANGULIZI
2. UTABIRI WA HALI YA MAJI
3. ATHARI
4. USHAURI
5. HITIMISHO

Bodi ya Maji Bonde la Wami/Ruvu imeandaa na kuwasilisha utabiri wa wingi wa maji katika Mto Ruvu kwa kuzingatia vituo vilivopo katika *Catchment* (**Kielelezo Na.1**) kwa kipindi cha kuanzia tarehe 6 Novemba hadi 16 Novemba, 2026. Utabiri huu unalenga kuwezesha wadau wa Mto Ruvu katika sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Ujenzi, Viwanda, Utalii na Mamlaka za Maji Safi na Usafi wa Mazingira kufahamu mwenendo wa wingi wa maji katika mto huo ili waweze kujua hali ya mwenendo wa wingi wa maji. Aidha, utabiri huu umezingatia utabiri wa hali ya mvua na Joto zilizotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA).




Kielelezo Na.1: Vituo vilivyotumika kufanya utabiri wa wingi wa Maji katika *Catchment* ya Mto Ruvu

2. UTABIRI WA HALI YA MAJI

Utabiri wa hali ya wingi wa maji katika Mto Ruvu umefanyika kwa siku kumi zijazo kuanzia tarehe 6 Novemba hadi 16 Novemba, 2026 kama inavyoonekana katika Jendwali Na. 1; -

Jendwali Na. 1: Utabiri wa hali ya wingi wa maji Mto Ruvu.

Jina la Mto	Utabiri wa Hali ya Wingi wa Maji	Kielelezo
Ruvu	Utabiri unaonesha kuwa wingi wa maji kwa sasa na siku 10 zijazo utaendelea kuongezeka kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha katika safu za Milima ya Uluguru ambayo ndiyo chanzo cha Mto Ruvu. Utabiri wa siku 10 zijazo unaonesha kuwa wingi wa maji utaongezeka na kuwa juu ya wastani ukilinganisha na wastani wa muda mrefu (2009–2024). Aidha, kiasi cha maji kilichopo kwa sasa na siku 10 zijazo kinatosheleza mahitaji ya wadau ya lita 6,000 kwa sekunde	

3. ATHARI ZINAZOWEZA TOKEA

Wingi wa Maji kwa sasa unaendelea kuongezeka kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha katika safu za milima ya Uluguru.

4. USHAURI KWA SEKTA MBALIMBALI

Bodi inapenda kuwashauri watumiaji wa Maji katika sekta ya Kilimo, Ujenzi, Madini, Utalii, Mifugo na uvuvi, Mamlaka na Wakala wa Maji Safi na Usafi wa Mazingira kuendelea kutumia kiasi cha maji kilichopo kwa ufanisi.

5. HITIMISHO

Bodi itaendelea kutoa taarifa ya mwenendo wa wingi wa maji kila baada ya siku kumi na kuwahabarisha watumiaji na Mto Ruvu ili waendelea kuchukua hatau za tahadhari dhidi ya kuongezeka/kupungua kwa wingi wa maji katika Mto Ruvu kwa siku zijazo.